# Sanaajadiiya Mtandaoni: Misimbo Ibuka Yaimarika ilhali Kiswahili Chaganda

*Peter Githinji*
*Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya*

**Ikisiri**

**Kama lugha nyinginezo, ubunifu ulioandamana na ngoma za jadi, mashairi, miiko, ngano na masimulizi mengineyo katika lugha ya Kiswahili ulididimia na sanaa hii ikagandama pale tanzu mbalimbali zilipoandikwa kwenye vitabu. Kiswahili kiliposambaa kutoka Uswahilini, hakikujumuisha kimamilifu sanaajadiiya ya tamaduni za wakaazi wa bara. Hivyo basi kumekuwa na haja ya uwiano kati ya sanaajadiiya ya Kiswahili na ile ya tamaduni nyinginezo. Makala haya yanauangaza msimbo ibuka wa Sheng na jinsi umekuwa kielelezo kizuri cha namna vipengele vya lugha ya Kiswahili vinaweza kufinyangwa upya na kuendelezwa ili kusawiri uhalisia wa watumizi wa lugha. Makala inadai kuwa Kiswahili kimeganda katika uwanja wa sanaajadiiya na nafasi yake kuchukuliwa na Sheng hasa katika matumizi ya TEHAMA. Tanzu nne za sanaajadiiya ya Sheng zitajadiliwa; mchongoano, ujinga ni…, methali, na uvumi. Makala haya yatajaribu kujibu maswali kama vile; Je, tanzu hizi ni upotovu wa nidhamu au ni sanaa yenye nafasi yake katika utagusano wa kijamii? na je, ni kwa kiasi gani tanzu hizi za sanaajadiiya zimefanikiwa kutekeleza majukumu yanayotekelezwa na sanaa kwa jumla? Makala yanapendekeza ukubalifu wa misimbo ibuka itakayowasilisha uhalisia wa mikatadha tofauti ya Kiafrika ili kukifanya Kiswahili kukubalika katika sehemu tofauti za Afrika.**

**Maneno Muhimu**: Sanaajadiiya, Sheng, Mchongoano, Methali, Fasihi Simulizi.

## Utangulizi

Mawasiliano ya kidijitali yameshamiri katika maisha ya kila siku miongoni mwa vijana ambao ndio washirika wakubwa mtandaoni na TEHAMA kwa jumla. Ni kawaida kuwaona vijana pamoja wakibofyabofya simu zao badala ya kuongea na wenzao walio karibu nao. Wabeuzi wa teknolojia hulalamika kuwa mtandao una athari hasi kwa mawasiliano baina ya watu huku wakikataa kukubali kuwa hii ni sura badilifu ya mawasiliano inayotokana na uhalisia wa maisha ya kisasa.

Kutokana na hali hii, kutathmini ni kwa kiwango gani mawasiliano ya kidijitali yanaiga mawasiliano ya ana kwa ana ni suala muhimu. Je, diskosi ambazo kwa kawaida zimerithishwa vizazi baada ya vizazi zikiwakilishwa mtandaoni zitakuwa zimehifadhi uhalisia au zitakuwa zimebadilika kiasi cha kupoteza uasilia wake? Mtandao huruhusu ubunifu wa kazi za sanaa ikilinganishwa na mawasiliano ya ana kwa ana? Katika kujibu maswali haya, makala haya yataangazia suala la ubunifu katika sanaajadiiya mtandaoni inayoendeshwa kwa masuala ibuka ya Sheng ikilinganishwa na Kiswahili sanifu. Vipera tofauti vya sanaajadiiya ambavyo hupatikana katika msimbo wa Sheng vitachambuliwa ili kuangazia jinsi Sheng imejitwalia vipengele fulani vya sanaa jadi ya Kiswahili na kuziingiza katika diskosi yake.

Kwa muda mrefu, sanaa ya jadi hasa ngano, methali, ushairi, nyimbo, na vitendawili imekuwa ikishughulikiwa katika fasihi simulizi. Kauli ambayo hujitokeza kila mara fasihi simulizi inapotajwa ni kuwa ni sanaa inayotambwa na ambayo hurithishwa vizazi kutoka kwa vizazi vilivyotangulia. Urithishaji huu hudhihirisha mwingiliano kati ya uhalisia wa enzi zilizopita na maisha ya siku hizi. Jambo hili linamfanya Ben-Amos (1971) kudai sanaajadiiya inaweza kuwa mvinyo wa zamani katika chupa mpya na pia mvinyo mpya katika chupa za zamani, lakini ni nadra sana kufikiriwa kama mvinyo mpya katika chupa mpya (uk. 5). Kauli hii ya Ben-Amos imebeba imani za wasomi wengi ambao hunasibisha sanaajadiiya na uzamani. Mwimbaji wa nyimbo za jadi, kwa mfano, huwa na uhuru wa kuzifinyanga upya kufuatia mazingira anamoimbia, lakini uzamani katika mtindo na muundo wa nyimbo hizo kwa kiwango kikubwa haubadiliki. Vilevile, hadithi moja ikisimuliwa na wasanii wawili inaweza kutofautiana kwa vipengele kadha wa kadha, lakini uzamani wa vipengele vya kimsingi haubadiliki. Jambo hili hutokana na urithishaji na urithishwaji wa ruwaza ambazo huitambulisha sanaa ya aina fulani. Hivyo basi, ukuruba kati ya uzamani na sanaa ya jadi ambao umeathiri mitazamo ya wasomi kwa muda mrefu ni jambo lisilopingika. Faukwa na hayo, mtazamo huu unakumbwa na changamoto tunapofikiria kuhusu misimbo ibuka ambayo huibua sanaa inayotofautiana na sanaa za lugha chagizi. Je, misimbo ibuka kama Sheng ambayo imeanza hivi karibuni ina nafasi yoyote ikiwa tutahusisha sanaajadiiya na uzamani? Vilevile, ikiwa sifa moja ya sanaajadiiya ni utambaji hasa ule unaohusikana na mawasiliano ya ana kwa ana, basi ni kwa kiasi gani tunaweza kuiita sanaa ya wazungumzaji wa Sheng sanaajadiiya wakati imetumika mtandaoni badala ya kutambwa?

## Sheng ni msimbo unaojisimamia au huganda kwenye Kiswahili?

Wataalam wengi wamedai kuwa Sheng iliibuka katika mitaa ya wafanyi kazi wa serikali katika jiji la Nairobi mnamo miaka ya sitini na sabini (Osinde, 1986; Spyropoulos, 1987; Mazrui, 1995; Abdulaziz na Osinde, 1997). Ni msimbo ibuka ambao kwa kiwango kikubwa hufuata muundo wa lugha ya Kiswahili huku

ukikopa maneno kutoka kwa Kiswahili, Kiingereza na lugha nyinginezo. Ni sifa hii iliyomfanya Githiora (2002) adai kuwa Sheng ni lahaja ya Kiswahili inayotumika na jamii za mjini. Hata hivyo, Sheng imedhihirisha tofauti mbalimbali kama vile sauti za ziada ambazo hazipatikani katika Kiswahili (Bosire, 2008) na vipengele vya kisarufi kama vile utumikaji wa ngeli ya KA/TU na uongezaji wa kiambishi MA katika baadhi ya nomino za ngeli ya U (Bosire 2008) ambavyo havipo katika Kiswahili sanifu. Zaidi ya hayo, maana ya baadhi ya maneno ya Kiswahili hubadilika maneno hayo yanapotumika katika muktadha wa Sheng. Vilevile, Sheng hukiuka baadhi ya kaida za kimatumizi za Kiswahili sanifu kimaksudi kwa minajili ya utambulisho (Kandagor, 2016). Hivyo basi, ijapokuwa Sheng haitofautiani sana na Kiswahili, ni kweli kuwa ni mfumo ambao huwa na kanuni zake ambazo si lazima zilingane na zile za Kiswahili sanifu.

Kutokana na hayo, tunaweza kujiuliza iwapo inawezekana mtu kuzungumza Sheng bila kutumia Kiswahili. Jibu litategemea mtazamo wa mtu kuhusu msimbo huu. Ikiwa tunazingatia sarufi ambayo Sheng imekopa kutoka kwa Kiswahili, basi jibu ni kuwa huwezi kuzungumza Sheng bila kuzungumza Kiswahili, hasa tukikumbuka mawazo ya Githiora (2002) kuwa Sheng ni lahaja ya Kiswahili cha mjini. Kwa upande mwingine, iwapo tutazingatia vipandesauti, kuwepo kwa ngeli ambazo hazipo katika Kiswahili, kutotii baadhi ya sheria za sarufi ya Kiswahili, na pia kubadilika kwa maana ya maneno, basi tunaweza kudai kuwa mtu anaweza kuzungumza Sheng bila kuzungumza Kiswahili. Mantiki ya madai haya yanatokana na ukuruba ulioko kati ya lugha mbalimbali zenye asili moja. Kikuyu na Kiembu kwa mfano zinakaribiana sana, lakini kushirikiana baadhi ya maneno na vipengele fulani vya kisarufi hakuwezi kutufanya kudai kuwa lugha hizi ni lugha moja bali tunazishughulikia kama mifumo miwili inayojitawala. Baadhi ya mambo ambayo hufanya lugha hizi zichukuliwe kuwa tofauti ni kuwa na mila na desturi ambazo ni tofauti. Mila na destuli huandamana na amali nyinginezo za kijamii mojawapo ikiwa sanaa, hasa sanaa za utambaji na uigizaji. Baadhi ya sanaa za kuigiza katika Kiswahili zimejitokeza katika Sheng, lakini ubunifu umezipa sura mpya katika diskosi ya Sheng.

### Je kuna sanaajadiiya katika msimbo wa Sheng?

Ikiwa Sheng imezungumzwa kwa tarkriban miaka sitini hivi, basi inawezaje kuwa na jadi? Na ikiwa haina jadi, basi inawezaje kuwa na sanaajadiiya? Mojawapo ya sababu ya kutumia istilahi sanaajadiiya ni kuwa tunahepa uhusishwaji wa dhana hii na uzamani. Kwa ufafanuzi bora zaidi dhana ya jadiiya (folk) hapa imechukuliwa kama watu wa kawaida kwa jumla ambao shughuli zao za kila siku hazitegemei uchambuzi wa namna ya kuishi kuegemea misingi ya kisayansi. Akina yahe wakipiga soga mitaani, marafiki wawili wakilumbana, au wazungumzaji wanapokaa chini na kufanyiana mizaha; ikiwa haya yanachukua sura ya kisanaa, yote yatajumuishwa katika fasiri ya sanaajadiiya. Kwa fasiri hii, basi ni wazi kuwa Sheng ina sanaajadiiya ambayo imechangiwa na Kiswahili kwa

kiwango kikubwa. Haya hutokea kupitia ukiukaji wa sheria za kimuundo na pia kaida za kijamii kuhusu matumizi ya lugha. Ukiukaji huu umeibua aina ya diskosi ambayo imekopwa kutoka kwa Kiswahili na lugha nyinginezo, lakini diskosi yenye upekee wake. Kiswahili na lugha nyinginezo zinazoshiriki ni maligafi ya sanaajadiiya ya Sheng. Hata hivyo, sio vipera vyote vya sanaajadiiya ya Sheng vina asili ya Kiswahili, jambo litakalodhihirika tukiangalia vipera vinne vya sanaajadiiya ya Sheng ambavyo ni methali, mchongoano, ujinga ni…, na uvumi. Kila kipera kitashughulikiwa kivyake.

**Methali za Kikenya**

Mulokozi (1986) ameshughulikia methali chini ya kipera cha semi ambacho hujumuisha methali, vitendawili, misimu, mafumbo na lakabu. Methali za Kikenya huwa methali za kawaida za Kiswahili ambazo hufuata ruwaza za methali zinazojulikana lakini baadhi ya maneno huondolewa na badala yake maneno ambayo hupotosha maana ya methali huchukua nafasi yake. Mifano ya methali za Kikenya ikiandamana na visawe vyake katika methali za kawaida za Kiswahili ni kama ifuatayo.

1) Mtaka cha rungu lazima achore saba
   *Mtaka cha mvunguni sharti ainame*
2) Mbio za sakafuni, huishia kwenye balcony ya Samuel Wanjiru
   *Mbio za sakafuni huishia ukingoni*

Methali hizi mbili zinatokana na methali za Kiswahili ambazo zimeundwa upya. Katika methali ya (1), *rungu* ni nomino ya kawaida ya Kiswahili, lakini katika Sheng, maana yake sasa imebadilishwa kumaanisha dhakari. *Kuchora saba* katika Kiswahili sanifu kunamaanisha kitendo cha kutumia kalamu kuandika alama ya nambari saba, lakini katika Sheng, nahau hiyo humaanisha kitendo cha kujiweka tayari ili utendewe tendo la ndoa (Ogechi, 2005). Hapa kuna ukiukaji wa kaida za kimawasiliano wakati methali ambayo kwa kawaida hutoa wosia wa kufanya kazi kwa bidii imebadilishwa kudokeza shughuli za ngono. Masuala ya ngono katika lugha ya Kiswahili huwa mwiko katika maongezi ya kawaida, na inapobidi yazungumziwe, basi tasifida hutumika. Hata hivyo, vijana watumiao Sheng hawajafungwa na miiko ya jamii ya Waswahili au mitazamo ya jadi kuhusu mapenzi na ndoa. Hivyo basi, mada hizi zinashughulikiwa kwa njia tofauti na kizazi cha siku hizi ikilinganishwa na kizazi cha awali. Isitoshe, methali hizi hupakiwa mitandaoni ambapo mwandishi hutumia lakabu akizielekeza kwa yeyote atakayezisoma akijua kwamba ukiukaji wa kaida za maongezi kuhusu miiko hautasutwa au kuadhibiwa. Katika methali ya (2), neno ukingoni limebadilishwa na "balcony ya Samuel Wanjiru" aliyekuwa mwanariadha mashuhuri katika mbio za masafa marefu. Inadaiwa kuwa aliaga dunia baada ya kuruka kutoka kwenye roshani ya nyumba yake. Samuel aliyeaga dunia 2011, alisemekana kuwa na sifa ya majivuno na tabia ya kuwatweza wengine kutokana

na utajiri wake. Tanzia yake imefanywa kuwa onyo kuwa kiburi huleta maangamizi. Ubadilishaji wa ukingoni na "balcony ya Samuel wanjiru" unaonyesha jinsi Sheng hutumia maudhui na matukio ya kawaida kusawiri uhalisia wa maisha katika methali hizi. Kwa vile ni mwiko kusherehekea kifo cha mtu yeyote, wasemaji wa Sheng, wanahepa kukaripiwa na jamii kwa sababu msimbo hupunguza makali ya semi zao.

Methali moja ya Kiswahili inaweza kuzua methali zingine kadha kama tunavyoona katika methali zifuatazo ambazo zote zimetoka kwenye methali hiyo moja ya "Mtaka cha mvunguni sharti aimane"

3) Mtaka cha mkunduni, ni father kei nzito

4) Mtaka cha father kizito, sharti abendover

5) Mtaka cha poko sharti achote

Mifano miwili ya (3) na (4) inahusu ulawiti, mada iliyotawala mijadala ya Wakenya kufuatia kashfa ya Padre Kizito aliyeshtakiwa kwa kuwadhulumu wavulana wadogo kimapenzi. Katika methali (3), *mvunguni* limebadilishwa na *mkunduni* kwa minajili ya kuhifadhi takriri, lakini pia tunapata jinsi Sheng hucheza na sauti za majina kwa kuliunda neno Kizito upya likawa *kei* nzito, yaani dhakari nzito. Ijapokuwa tuhuma dhidi ya Padri Kizito zilitupiliwa mbali kwa kukosa mashiko, jamii bado ilimwona kama mlawiti. Methali ya (4) inamrejelea anayelawitiwa, lakini hapa anaonekana kama anashiriki kitendo hiki kwa hiari. Anayetaka kutendewa kitendo hicho na Padri Kizito, basi, sharti ainame. Kitendo cha kuinama kimehifadhiwa, lakini kwa lugha ya Kiingereza. Methali ya (5) ni tofauti kidogo kwa vile sasa inaashiria uasherati miongoni mwa vijana. Anayetaka huduma za kahaba, ni lazima alipe. Methali hizi zote zimeunganishwa na jambo moja. Zote zinahusu ngono, mada ambayo si kawaida kutokea kwenye mazungumzo ya ana kwa ana katika Kiswahili sanifu. Hivyo basi kuwepo mtandaoni kunawapa washiriki uhuru wa kuibadilisha wapendavyo. Vilevile, wanaweza kuzungumzia mambo ambayo ni mwiko kwa sababu hamna hatari ya kuadhibiwa. Ni muhimu kutaja kuwa methali hizi hazijifungi katika masuala ya ngono tu, lakini hata mada nyinginezo kama tunavyoona katika mifano ya (6) na (7).

6) Panapo Kivuitu hapakosi wizi wa kura
   *Panapo moshi hapakosi moto*

7) Asiyekubali kushindwa atakuwa PM
   *Asiyekubali kushindwa si mshindani*

Marehemu Kivuitu alikuwa Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi nchini Kenya kati ya 1997 hadi 2008. Isipokuwa uchaguzi wa 2002, chaguzi zingine zote zilikumbwa na tuhuma za wizi wa kura, jambo ambalo limewafanya wazungumzaji wa Sheng, wengi wao wakiwa vijana kumnasibisha Kivuitu na

wizi wa kura. Methali ya (7) inamdhihaki Waziri Mkuu wa zamani Raila Odinga. Ijapokuwa baadhi ya Wakenya huamini kuwa uchaguzi mkuu huibiwa mara nyingi, jambo ambalo humpokonya Raila uongozi, kuna kundi jingine linaloamnini kuwa hajawahi kushinda hata mara moja na kila mara imekuwa kawaida kwake kulalamika kwamba uchaguzi umeibiwa. Kutokana na hayo, amesawiriwa na methali hii kama mshindani ambaye hakubali kushindwa, lakini methali inaendelea zaidi kuonyesha kuwa hata kama hujashinda, uking'ng'ania kuwa umeshinda, unaweza kuzawadiwa na cheo kikubwa. Methali za Kiswahili ambazo wazungumzaji wa Sheng wamezibuni upya ni nyingi na zinaashiria ushirikiano katika diskosi ambapo wanadhihirisha ubunifu wao mtandaoni.

### Mchongoano

Mchongoano ni 'malumbano ya utani' (Momanyi, 2017) na hushughulikiwa sawia na kijipera cha ucheshi katika fasihi simulizi. Mchongoano haupo katika Kiswahili sanifu, lakini una mwangwi katika fasihi simulizi ya jamii mbalimbali za Kiafrika na pia Waamerika wenye asili ya Afrika (Githinji, 2006; 2011). Uigizaji wake au muundo wake unafanana na vipera vya fasihi simulizi kama vile vitendawili (Kihara, 2013) kutokana na kuwepo kwa anayechongoa, anayechongolewa na hadhira. Hata hivyo, sio lazima mchongoano ufanyikao mtandaoni uwe na mlengwa au hadhira. Ijapokuwa mchongoano haupo katika fasihi ya Kiswahili, una nakili yake katika utanzu wa utani katika fasihi simulizi na ulitekeleza dhima maalum katika jamii. Kwa mujibu wa Momanyi (2017, uk 1) utani ulikusudia kufundishana maadili ya kijamii, kuelimishana, kukosoana au hata kufunzana kuelekezana. Utani hutumika katika miktadha mbalimbali kama vile arusini, kazini na hata matangani.  Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, (Kezilabahi, 1971), Zakaria aliuawa katika mazishi ya mtani wake alipowaudhi waombolezaji walioudhika na utani wake katika sherehe yenye huzuni. Katika sherehe nyingi, ni dhima ya wafawidhi kufanya mizaha ili kuifurahisha hadhira iliyohudhuria.

Katika uigizaji wa ana kwa ana, mchongoano hujumuisha wahusika wawili ambao wamezoeana na wanajuana vizuri. Mhusika mmoja hutoa kauli yenye kumsuta mwenzake lakini yenye ucheshi, naye mhusika wa pili hutumia ubunifu wake kujibu huku akizingatia mada aliyoanza nayo mwenzake (Labov, 1972). Ifuatayo ni mifano ya mchongoano ikitafsiriwa kwa Kiswahili sanifu;

1) Budako fala alirepeat kuzaliwa
   *Baba yako ni mjinga alirudia kuzaliwa*
2) Mathako ana rasa square
   *Mama yako ana matako ya mraba*

Kama tunavyoona katika (1), hakuna mtu anayeweza kuzaliwa mara mbili, kwa hivyo, kauli hii si upotoshi, lakini ni utani ambapo anayelengwa habidiki kukanusha. Vilevile katika (2), hakuna mtu ambaye ana matako ya mraba. Ni kule

kutia chuku kwa mambo yasiyowezekana ambako kunaifanya fani hii kuruhusu upuuzi unaonuia kuzua ucheshi tu. Mada za mchongoano zinaweza kuhusu watu wa familia, sura ya mtu, ujinga wa mtu, mifugo, wanyama wanaowekwa nyumbani, mali ya familia na kadhalika kama tunavyooka katika mifano inayofuata.

3) Radio yenu ni mzee mpaka inaplay v.o.k
*Radio yenu ni ya zamani sana hivi kwamba huonyesha vipindi vya Sauti ya Kenya*
4) Paka yenu noma mpaka ikishika panya inaitisha chumvi
*Paka wenu ni mlimbwende hivi kwamba akishika panya huitisha chumvi*
5) Ati uko na macho so mpaka moja inaona ingine
*Ati una macho makubwa hivi kwamba jicho moja huona jingine*
6) Ati we ni mshort mpaka we hupeleka panadol ka tyre
*Ati wewe ni mfupi hivi kwamba huzungusha panadol kama tairi*
7) Manzi yako hukuwa na miguu mbili za left
*Mpenzi wako huwa na miguu miwili ya kushoto*
8) Hao yenyu ndogo mpaka dining room iko nje
*Nyumba yenu ni ndogo hivi kwamba chumba cha kulia kiko nje*

Kwa kiwango kikubwa, sanajadiiya ni sanaa ya mazungumzo na uigizaji. Akilinganisha vitendawili na mchongonao, Kihara (2013) anadai kuwa kuna sifa ambazo tanzu hizi mbili zinashirikiana kama vile kutoa ombi la kutega kitendawili au kuchongoa mwenzake. Vitendawili huisha anayetegewa akishindwa kutegua na kuombwa apeane mji kabla ya kuambiwa jibu ilhali mchongoano huisha mshiriki moja anaposalimu amri au kusutwa na wenzake asalimu amri. Hivyo basi, sanaa ya aina hii inayohusu uigizaji huhitaji angalau wahusika wawili au mhusika mmoja na hadhira. Hata hivyo, sanaajadiiya siku hizi imevuka mipaka ya mazungumzo kutokana na maendeleo ya kiteknolojia. Katika majarida, vitabuni, magazetini na mtandaoni, mchongoano unaweza hata kushirikisha mhusika mmoja na hadhira dhahania. Kupitia mchongonao tuonaona jinsi sanaa ya jadi imeumbwa upya na kuwa sanaajadiiya ya watumiaji wa msimbo ibuka wa Sheng.

**Kukejeli ujinga katika utani wa "Ujinga ni…"**

Ucheshi unaokejeli ujinga ni kipera kingine cha sanaajadiiya ya watumiaji wa Sheng na hudhamiria kuonyesha upuzi au upumbavu wa kushikilia imani fulani au kufanya vitendo fulani. Fani hii hushirikisha imani maarufu zinazoshikiliwa na jamii, mara nyingi zikiwa usaguzi. Imani hizi kwa kawaida huwa potofu, lakini muradi tu Wakenya wengi wamezishikilia, basi zinatumika katika sanaa hii. Tuchukue mfano wa "Ujinga ni kupeleka slimpossible Turkana" kwa mfano.

*Slimpossible* ni shindano lililokuwa kwenye runinga ya *Citizen* ambapo watu wanene walishindana kupunguza uzani. Lengo la slimpossible lilikuwa kuboresha afya ya watu wenye uzani mkubwa kupitia lishe bora na mazoezi. Jamii ya Waturkana ina sifa ya kuwa na watu wembamba. Ikiwa watu wanene ndio waolengwa, basi kupeleka shindano kama hili kwa watu wembamba ni upumbavu kwa sababu halitasaidia kwa lolote. Mifano mingine ni kama ifuatayo

1) Ujinga ni nurse kuamsha mgonjwa ameze dawa za kulala
2) Ujinga ni kureduce volume ya TV ndo usome sms
3) Ujinga ni kuambia kiwete akanyagie stori
4) Ujinga ni kudhani first born wa mama mboga anaitwa mboga

Kumwamsha mgonjwa ili umpe dawa za kulala ni upeo wa ujinga kama tunavyoonyeshwa na mfano (1). Katika mfano (2), kusoma ujumbe wa simu hakuhitaji mtu kuzima televisheni au kupunguza sauti na mtu afanyaye hivyo hudhihirisha ujinga wa kutotambua kuwa kelele kutoka kwa televisheni haziwezi kuzuia mtu kusoma ujumbe wa simu. Kumekuwa na malalamiko mengi kuwa vijana wa siku hizi hawana umakinifu kwa sababu badala ya kusikiliza, wako kwenye simu wakibofyabofya. Hili ni jambo ambalo bado halijadhibitishwa na utafiti, lakini vijana hawa wamezoea kushughilikia mambo mengi kwa wakati mmoja. Kukitokea jambo kwa ghafla, huacha simu zao na kushughulika ipasavyo. Haya ni mabadiliko ambayo yametokea katika tabia za vijana kukabiliana na ulimwengu changamano. Mfano (2) unahakiki jamii inayoshikilia uzamani kuwa ni lazima ufanye jambo moja kwa wakati mmoja. Vijana husikiliza na pia kutumia simu kwa wakati mmoja. Fasiri ya mfano (3) inatokana na neno ‘kanyangia’ ambalo katika Sheng humaanisha kutosema au kuficha habari fulani. Kiwete hana miguu, kwa hivyo hawezi kamwe kukanyanga na kumwambia akanyangie chochote ni ujinga. Ukinzani kati ya maana halisi na maana ya kijazada ndio unaozua ucheshi. Mfano wa mwisho unaakisi utamaduni wa Kiafrika ambapo wazazi huheshimiwa kwa kuitwa mama au baba ya watoto wa kwanza. Katika Sheng mama mboga ni jina la kikazi analopewa mwanamke yeyote anayeuza mboga na halina uhusiano wowote na uzazi au watoto.

Utani wa aina hii ni tofauti na kijipera kingine ambacho ni aina ya masimulizi yanayoitwa “mimi sipendi ujinga” au “*x* hapendi ujinga”, ambapo *x* husimamia nomino katika nafsi yoyote. Masimulizi haya ya kubuni kwa kawaida huwa mafupi, mara nyingi kati ya sentensi moja na sentensi nne. Msimulizi husimulia kuhusu tatizo fulani kisha huelezea werevu uliotumika kutatua tatizo hilo na mwishowe kumalizia kwa kauli “mimi sipendi ujinga” au “x hapendi ujinga”. Hebu tuangalie mfano wa utani wa aina hii.

> Sa juzi nimecall crush wa me, kiboy kikapick na kikaanza kuniuliza maswali ati we ni nani, mbona unacall dame yangu, me nikamjibu ‘naitwa Kimani doctor yake mwenye simu, aliniambia niwe namcall

kumkumbusha akunywe ARV zake, mazishi ya huyo boy ni sato, sipendi ujinga mimi.

Katika kisa hiki, mvulana anapopata msichana anayemtamani tayari ana mpenzi, anavuruga uhusiano huo kwa kutoa habari za uongo. Anamdanganya mpenzi wa msichana kuwa msichana hutumia dawa za UKIMWI, jambo linalosababisha mvulana kufa kwa kushtuka kuwa tayari ameambukizwa. Tofauti na ule ucheshi wa awali unaokejeli ujinga, huu wa "sipendi ujinga" hauonyeshi upuzi au ujinga kwa upande wa wahusika wanaozungumziwa, ni majigambo ya aina fulani ambayo yanafanana na vifugo (Mulokozi, 1986), lakini hayana upevu jinsi Mulokozi amefafanua. Utani mwingine wa "sipendi ujinga" unachukua sura ya majibizano yanayotumia kitendawili kama huu;

| | |
|---|---|
| Mwalimu: | Kitendawili? |
| Mimi: | Tega |
| Mwalimu: | Nyumba yangu haina mlango |
| Mimi: | Ita fundi. Stakangi ujinga mimi. |

Mwalimu anatega kitendawili cha kawaida, lakini mwanafunzi anakifanya mzaha kwa kukitoa katika muktadha wa sanaa na kukiingiza katika uhalisia ili kujigamba kwa werevu wake. Tunaweza kulinganisha kitendawili hiki na kauli za kuonyesha ujinga kama vile "ujinga ni mwalimu kumwambia mwanafunzi kuwa nyumba yake haina mlango badala ya kuita fundi". Ikiwa kufanya hivyo ni ujinga, basi mwanafunzi anajifanya jasiri kwa kutoa kauli kuwa yeye hapendi ujinga.

**Uvumi na uthibitisho katika kipera cha "Ati…, kwani…"**

Sawia na utani wa "*ujinga ni…*" ambao huwa hoja fupi fupi, utani wa *ati…kwani* huchukua muundo wa kauli na swali. Sehemu ya kwanza ambayo mara nyingi huanza na neno "ati" huwa kauli ya uvumi unaoelezea hoja au habari fulani ambazo hazijadhibitishwa. Sehemu ya pili huwa swali kuhusu uvumi huo kwa kusaili mantiki yake. Utani hutokana na swali linalokosoa hoja iliyotolewa katika sehemu ya kwanza. Aidha, hutoa jazada ambazo huakisi imani za kijamii au usaguzi. Pia sehemu ya pili huwa imepigwa chuku, jambo ambalo huifanya hadhira kufasiri utani huu kwa kuhoji uhusiano uliopo kati ya sehemu ya kwanza na ya pili. Hebu tutazame mifano ya utani katika kipera hiki.

1) Ati chips 200, kwani waiter anakam akiwa chips funga
2) Ati unafunga choo na padlock, kwani kuna mwizi wa shonde?
3) Ati success card ni 400, kwani ina mwakenya
4) Ati sabuni 200, kwani inaosha dhambi
5) Ati carpet 20,000/-, kwani ni ya Aladdin?

Katika (1) hamna mantiki ya kununua chipsi kwa shilingi mia mbili, badala ya bei ya kawaida ya shilingi mia moja ikiwa hakuna nyongeza ya aina fulani. Utani umejikita katika dhana ya "chips funga" (msichana anayechukuliwa na mwanamume aghlabu katika sehemu za starehe kwa nia ya ngono). Thamani ya shilingi mia mbili ya chipsi itarazinishwa ikiwa mhudumu atakuwa nyongeza ya zile chipsi za kawaida kwa mnunuzi. Tabia ya kufunga choo na kufuli inadhihakiwa katika (2) kwa sababu hakuna mtu mwenye akili timamu anaweza kuiba takamwili.

Mada zinazojitokeza katika utani huu zinaonyesha kuwa wanaozibuni huzingatia masuala yanayoakisi maisha ya kila siku na changamoto zinazowakumba vijana. Jambo hili linajitokeza wazi katika (3) ambapo tabia ya kutuma kadi za heri hasa wakati wa kufanya mitihani imeingizwa. Kadi zenye thamani kubwa zinakejeliwa kwa sababu haziwezi kumsaidia mwanafunzi kupita mtihani. Bei ya juu ya kadi inaweza kurazinishwa tu ikiwa itakuwa na maandishi haramu ambayo yanaweza kumsaidia mwanafunzi kuibia mtihani.

Maudhui ya bei pia yanaendelezwa katika (4) na (5). Ijapokuwa kuna sabuni ambazo huuzwa kwa bei ya juu, Wakenya wengi, hasa kutoka mitaa ya vibanda na sehemu nyinginezo ambazo jamii zenye mapato madogo huishi hutumiwa kufulia na pia kukoga. Kutumia sabuni ya shilingi mia mbili hakuwezi kuwa na mantiki iwapo sabuni hiyo haifanyi zaidi ya kusafisha nguo na mwili, kama vile kusafisha dhambi za mtu. Bei ya zulia ndiyo mada katika (5). Katika mitaa ya watu wa mapato madogo, nyumba nyingi hazina mikeka seuze sakafu. Hivyo basi, mazulia ya bei za juu huwa ni kama ndoto au hekaya kama zile za Alladin. Vilevile, thamani ya juu kiasi hicho kwa zulia itarazinishwa iwapo zulia hilo litakuwa la kimiujizamiujiza kama lile la Alladin.

Kuna vipera vingine vya sanaajadiiya ya Sheng kama vile utambaji wa hadithi kama alivyogusia Samper (2003) kuhusu 'mastoro' (hadithi) na masimulizi ya visa vya tajriba za kibinafsi (Githiora 2003), mitindo ya mavazi, salamu na maagano na kadhalika miongoni mwa vingine ambavyo havijashughulikiwa katika makala haya. Licha ya hayo, vipera hivi vine ambayo vimeshughulikiwa ni ushahidi tosha kuwa sanaajadiiya mtandaonio katika msimbo ibuka wa Sheng ni hai, kinyume na hali ilivyo katika Kiswahili ambacho kimekuwepo kwa mda mrefu zaidi. Hakuna maelezo mazuri ambayo yametolewa kuhusu kutoimarika kwa sanaajadiiya ya Kiswahili mtandaoni.

**Kugandama Kwa Sanaajadiiya ya Kiswahili mtandaoni**

Matumizi ya Kiswahili mtandaoni yameimarika kadri TEHAMA imezidi kuimarika. Kuna programu za redio na televisheni, blogu za kibinafsi, tovuti, mitandao ya kijamii, makamusi na mafunzo ya lugha na utamaduni. Pia kuna blogu zinazoelezea maisha na utamaduni wa Waswahili kama vile http://www.glcom.com/hassan/ ambayo ina mafunzo ya lugha, mashairi na

maelezo kuhusu kanga. Hata mashairi maarufu ya Kiswahili kama vile *Al Inkishafi*, *Mwanakupona* na *Fumo Liyongo* yanapatikana katika mtandao. Kuna pia vitendawili, methali na vijipera vingine vya fasihi simulizi vinavyopatikana mtandaoni. Licha ya haya, ni wazi kuwa sanaajadiiya ya Kiswahili imeganda mtandaoni kwa kukosa mwendelezo na uhuishaji. Kama tulivyodai awali, sanaajadiiya haipaswi tu kuiga uzamani, lakini inahitaji kutumia kaida za vipera vya jadi huku ikizifinyanga upya ili kusawiri uhalisia hai wa jamii husika. Hili lisipotendeka, vijana ambao ndio washiriki wengi mtandaoni hujipata wamekengeushwa na sanajaadiiya ya Kiswahili wanayoipata mtandaoni kwa vile haiwakilishi uhalisia wa maisha yao ya kila siku. Hili linatokana na kuwa sanaajadiiya ya Waswahili ilichochewa na mazingira na uhalisia wa jamii ya pwani, lakini Kiswahili kiliposambaa bara, uhalisia wake haukufungamana na ule wa pwani. Hii ikawa mojawapo ya sababu ya kugandama kwa sanaajadiiya ya Kiswahili, hasa kwa vijana.

Vijana hawa pia huwa ndio watumiaji wa wakubwa wa Sheng na uundaji upya wa sanaajadiiya ya Kiswahili huwa kama njia kuimarisha sanaa ya kimawasiliano katika msimbo wao huku ikiboresha mshikamano wa watumizi wa msimbo huu. Vilevile, ni muhimu kutambua sanaajadiiya ya lugha yoyote ile, Kiswahili kikiwemo kwa kiwango kikubwa huendelezwa kwa lugha msimbo ambao bado haujasanifishwa. Hiyo basi, sanaajadiiya ya Kiswahili ilikuwa hai wakati Kiswahili kilikuwa bado hakijasanifishwa. Jambo hili linadhihirika tunapozingatia vipera mbalimbali vya fasihi simulizi ya Kiswahili ambavyo vinapatikana katika lahaja mbalimbali za Kiswahili. Tenzi, visa asili, nyimbo na mashairi yalianza wakati Kiswahili kilikuwa bado hakijasanifishwa. Usanifishaji wa Kiswahili katika karne iliyopita uliathiri pakubwa ubunifu katika sanaajadiiya ambayo haikuwa tena sanaa hai, bali uradidi wa uzamani. Zaidi na hayo, baadhi ya vipera vya sanaajadiiya viliandikwa kwenye vitabu na masharti ya hakimiliki yakaathiri uundaji upya wa sanaa ya jadi. Sheng, kama msimbo ibuka unaobadilika ulikuja kujaza pengo hili na ukawa chombo muhimu cha kuendeleza sanajadiiya.

## Hitimisho

Katika kuhitimisha, ni muhimu kukubali kuwa ijapokuwa Kiswahili kimepiga hatua kubwa mtandaoni, Kiswahili sanifu hakijasaidia kuimarisha vipera vya sanaajadiiya mtandaoni. Tukizingatia kauli kuwa sanaajadiiya huendelezwa na lugha zisizo sanifu, Kiswahili hakina budi ila kujitwalia diskosi zinazoendeshwa kwa misimbo ibuka ili kuhakikisha kuwa nacho hakiachwi nyuma katika uwanja wa sanajadiiya. Misimbo ibuka kama Sheng nchini Kenya, Swahinglish na lugha ya mtaa nchini Tanzania ni viungo vya lugha ya Kiswahili. Hatua hii ya kupanua rahamu ya Kiswahili kutakuwa hatua muhimu inayorutubisha Kiswahili na pia kukifanya kukubalika katika mapana mapana zaidi. Jambo hili litakuwa muhimu hasa Kiswahili kinavyozidi kusambaa barani afrika na kwingineko. Vijipera

mbalimbali ambavyo Kiswahili hakikuwa navyo vitajitokeza jinsi Kiswahili kitaendelea kutumika na watumizaji wenye tamaduni ambazo ni tofauti na zile za afrika Mashariki. Kiswahili kitarutubika kwa kukubali vijipera hivi kama njia ya kukuza sanaa ya Kiswahili duniani. Matumizi ya Sheng mtandaoni yameonyesha kuwa lugha za Kiafrika zinaweza kuwa maligafi yanayoweza kuzalisha na kuimarisha sanaajadiiya ambayo inaakisi uhalisia wa jamii tumizi.

## Marejeleo

Abdulaziz, M. and K. Osinde. 1997. Sheng and Engsh: Development of a mixed code among the urban youth in Kenya. *International Journal of the Sociology of Language 125:43-63*

Ben-Amos, D. (1971).Toward a Definition of Folklore in Context. *The Journal of American Folklore, 84 (331), 3-15*

Bosire, M. (2008) Sheng, the Phonology, Morphology and Social Profile of an Urban Vernacular. State University of New York, Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa)

Githiora, C. 2002. Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? *Journal of African Cultural Studies*, 15: 2, 159-181.

Githinji, O. (2011). Insults and Folk Humor: Verbal Transgression in Sheng's Mchongoano. Festschrift in Honor of David Dwyer. *Joy of Language*, East Lansing, Michigan State University, https://www.msu.edu/%7Edwyer/JOLIndex.htm.

Githinji, P. (2007). *Mchongoano* Verbal Duels: A Risky Discourse. In Njogu, K. & Oluoch–Olunya, G. (eds.). (2007). *Cultural Production and Social Change in Kenya: Buildingbridges. Art Culture & Society*. 1. 89-109.

Kandagor, M. M. (2016). Vijana na Mawasiliano ya Rununu. *Katika Kiswahili na Maendeleo ya Jamii*. (Wahr. Mukuthuria, M., Ontieri, J., Kandagor M. M. na Sanja, L.). Dar-es-Salaam: TUKI.

Kezilabahi, E. (1988). *Rosa Mistika*. Dar Es Salaam. Dar es Salaam University Press

Kihara, P. (2013). On *Mchongoano* and Riddles in Kenya. *The Journal of Pan African Studies, 6, 6, 100-121.*

Labov, W. (1972). *Language in the Inner City; Studies in Black English Vernacular.* Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Mazrui, A. (1995). Slang and Codeswitching: The Case of Sheng in Kenya. *Afrikanistische Arbeitspapiere 42 168-179*

Mulokozi, M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi. *Mulika.2, 1-24*

Momanyi, C. (2017) Malumbano ya Mchongoano: Je, Huchongoa au Kudumaza Watoto Kielimu na Kimaadili? *Mulika;36, 1-7.*

Ogechi, N. (2005). The Language of Sex and HIV/AIDS among University Students in Kenya. In *Stichproben. Wiener Zeitschrift für kritische Afrikastudien* 9, 5, 123-149.

Osinde, K. (1986). *Sheng: An Investigation into the Social and Structural Aspects of an Evolving Language*. Chuo Kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).

Samper, D. (2002). *Talking Sheng: The Role of a Hybrid Language in the Construction of Identity and Youth Culture in Nairobi Kenya*. Chuo Kikuu cha Pensylvania, Tasnifu ya Zamifu (Haijachapishwa)

Spyropoulos, M. (1987). Sheng: Some Preliminary Investigations into a Recently Emerged Nairobi Street Language. *Journal of the Anthropological Society of Oxford, 18: 1,125-136*.